## Maswali

1. Kornelio alikuwa nani?
2. Kornelio alikuwa mtu mzuri. Alitakiwa afanye nini tena ili apate kuokoka?
3. Malaika aliambia Kornelio afanye nini?
4. Petro aliona ndoto gani?
5. Hiyo ndoto ilifundisha Petro nini?
6. Mungu aliambia Petro afanye nini watu kutoka kwa Kornelio walipokuja?
7. Petro aliambia nini Kornelio na jamii yake na marafiki zake?
8. Nini ilifanyika wakati Petro alikuwa bado anazungumza?
9. Petro aliwambia wafanye nini?
10. Inajalisha tunatoka kwa kabila gani au rangi au asili gani?

## Majibu

1. Kornelio alikuwa askari wa Kirumi.
2. Alitakiwa ajifunze juu ya Yesu, aamini, atubu na abatizwe.
3. Malaika alimwambia atume watu Yafa na wamlete Petro.
4. Aliona shiti imejaa wanyama wachafu ikitelemshwa chini kutoka Mbiguni. Aliambiwa akule wale wanyama wachafu. Alipokataa, Mungu alimwambia asiite kitu chochote najisi hali Mungu amekitakaza.
5. Mungu anapenda watu wote. Kila mtu anaweza kuwa na tumaini la wokovu katika Yesu.
6. Mungu alimwambia Petro aende nao.
7. Petro aliwambia juu ya Yesu Mwana wa Mungu.
8. Mungu alipea Kornelio Roho Mtakatifu, hata na kwa jamii yake na marafiki pia.
9. Mungu alikuwa amewaita wawe Wakristo. Lazima wabatizwe.
10. Hapana. Mungu anaita watu wote waokoke baada ya kubatizwa katika Kristo.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 2 Mwaka wa 2**

# 93 Kornelio


### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 10 na 11

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba upendo wa Mungu ni wa kila mtu, haijalishi kabila, rangi au asili ya mtu

### Somo



Kornelio alikuwa Mrumi. Alikuwa askari. Kornelio alikuwa Nahodha wa askari mia moja wa Kirumi. Alikuwa mtu wa maana kwa jeshi la Kirumi. Kornelio aliishi Kaisaria.

Kornelio alikuwa mtu mzuri. Alikuwa amejifunza juu ya Mungu. Alipenda Mungu na aliomba kila mara. Kornelio alikuwa mzuri kwa watu maskini.

Kornelio alikuwa mtu mzuri. Alipenda Mungu. Lakini kulikuwa na kitu kimoja cha mhimu alitakiwa afanya ili apate kuokoka. Mungu alimwonyesha kwamba lazima ajifunze juu ya Yesu Kristo, aamini Yesu, atubu na abatizwe.

Siku moja Kornelio alikuwa anaomba Mungu. Kwa maono aliona malaika wa Mungu akimwita. Malaika aliambia Kornelio atume watu Yafa. Malaika alimwambia kwamba hao watu watafute Petro. Petro alikuwa anaishi pwani kwa nyumba ya Simoni mtengenezaji wa ngozi. Hao watu walitakiwa wamlete Petro kwa nyumba ya Kornelio. Haraka sana Kornelio alituma watu watatu Yafa kwenda kuita Petro. Walisafiri haraka iwezekanavyo. Walifika Yafa siku iliyofuata.

Petro alipanda darini kwa nyumba ya Simoni. Alikuwa anaomba Mungu. Ilikuwa wakati wa chakula cha jioni kwa hivyo alikuwa na njaa. Alipokuwa bado darini, alijisikia kulala. Mungu akamwonyesha ndoto isiyo ya kawaida.



Petro aliona shiti ikiteremka chini kutoka mbinguni. Shiti hiyo ilifungwa pembe zote nne. Ilipofunguliwa, Petro aliona kwamba ilikuwa imejaa wanyama. Wanyama wote walikuwa wanyama wachafu – hawa wanyama walikuwa ni wale Wayahudi hawakuruhusiwa kukula. Petro alisikia sauti ikimwamrisha, “Inuka Petro, uchinje na ule.”

Petro aliudhika sana. Hakukuwa amekula kitu chochote chenye sheria ya Wayahudi ilisema kwamba ni chafu. Petro alijibu, “Siwezi kula hawa wanyama. Sijawahi kukula wanyama najisi.”

Mungu alimwambia Petro, “Usiite kitu chochote chenye Mungu ametakasa kwamba ni kichafu.” Hiyo ndoto ilionekania Petro mara tatu. Shiti hiyo ilirudi Mbinguni.

Wakati huo watu kutoka kwa Kornelio walifika kwa nyumba ya Simoni. Walitaka kumwona Petro.

Mungu alimwambia Petro, “Watu watatu wako wanakutafuta. Inuka na uteremke chini. Enda na hawa watu kwa sababu nimewatuma.”

Kornelio na hawa watu walikuwa Wataifa. Hawakukuwa Wayahudi. Wayahudi walijua kwamba Wataifa ni watu wachafu. Hawakushukulika na kitu chochote chao. Hawangeingia kwa nyumba ya Mtaifa. Hapo Petro akaelewa maana ya ndoto zake. Mungu alikuwa anaonyesha Petro kwamba katika Yesu, Mataifa wanaweza kuokoka.

Kesho yake Petro na wale watu watatu walienda Kaisaria. Kornelio alikuwa amewaongoja. Aliwakaribisha kwa nyumba yake. Petro hakukuwa ameingia kwa nyumba ya Mtaifa. Petro akakumbuka ndoto zake na mafundisho ya ujumbe wa Mungu. Alienda kwa nyumba na Kornelio. Petro alipata jamii ya Kornelio pamoja na marafiki wake. Walikuja kusikiliza maneno yenye Petro alikuwa nayo.

Petro aliwambia juu ya Yesu. Aliwambia yote yenye Yesu alifundisha. Aliwambia kuhusu miujiza yenye Yesu alifanya. Petro aliwambia kwamba Yesu Mwana wa Mungu, alikufa msalabani kuokoa watu kutoka dhambini. Baada ya siku tatu Yesu alifufuka tena. Mtu yeyote akiamini katika Yesu ataokoka.

Petro alikuwa bado anazungumza na Roho Mtakatifu ikashukia kila mtu aliyekuwa akisikiliza. Wayahudi Wakristo walishangaa kuona Mungu amewapa watu Wataifa Roho yake Mtakatifu.

Petro alikumbuka ndoto yake. Alijua kwamba Mungu anapenda watu wote. Haijalishi mtu ni wa kabila gani au rangi au asili yake. Kupitia kwa ubatizo katika Yesu, watu wote wana nafasi ya kuokoka.

Petro alisema kwamba Mungu amewapa Kornelio na Jamii yake Roho Mtakatifu. Inamaanisha Mungu amewaita kuwa Wakristo. Petro alisema lazima wabatizwe katika jina la Yesu. Kwa hivyo wote walibatizwa. Na kwa Mataifa yote walikuwa watu wa kwanza kuitwa Wakristo.